

## KIGOMA GRAND HIGH SCHOOL



### Mkoa wa Kigoma kumaliza tatizo la upugufu wa shule za mchepuo wa Sayansi kidato cha tano

**M**radi wa ujenzi wa ‘Kigoma Grand High School’ unatekelezwa katika Halmashauri ya Mji wa Kasulu, katika kata ya Msambara .

Ujenzi wa shule ya ‘Kigoma Grand High School’ ambao kwa wastani umefikia katika hatua ya ukamilishaji.

Utekelezaji wa mradi huu unalenga kutatua kero ya ukosefu wa shule za Masomo ya Michepuo ya Sayansi Mkoani Kigoma.





*Ujenzi wa  
Vyumba vinne  
(4) vya madara-  
sa ukiwa katika  
atua ya ukami-  
lishwaji tayari  
kwa kuanza ku-  
tumika mapema  
Januari, 2018.*

Kigoma Grand High School' inatarajiwa kufunguliwa rasmi kwa kuingiza wanafunzi wa kidato cha kwanza mwezi Januari, 2018 kwa wanafunzi wenye alama za juu za ufaulu, mwezi Julai, 2018 Wanafunzi wa kidatocha Tano kwa masomo ya Sayansi

*Mabweni mawili  
ya wanafunzi 48  
kila moja  
yamefikia hatua ya  
ukamilishaji.  
Mabweni mawili  
ya wanafunzi 80  
kila moja yapo  
katika hatua ya  
upandishaji wa  
ukuta.*





## MIKAKATI YA UANZISHWAJI WA BENKI YA WANANCHI KIGOMA KUZAA MATUNDA



**Mkuu wa Mkoa wa Kigoma Mhe. Brigedia Jenerali (mst.) Emmanuel Maganga akitoa maelekezo kwa kikosi kazi kinachoshughulikia uanzishwaji wa Benki ya Wananchi Mkoani Kigoma Kushoto kwake ni Katibu Tawala wa Mkoa Bw. Carles Pallagyo na kulia I Bw. Ramadhan Gange Mweyekiti wa TCIA Kigoma**

**M**chango wa sekta binafsi kwa kushirikiana na serikali ni pamoja na wadau mbalimbali wa maendeleo, chachu kubwa ya maendeleo katika kufanikisha dira ya serikali ya nchi ya viwanda na kufikia uchumi wa kati.

Amesema Mkuu wa Mkoa wa Kigoma Brigedia Jeerali Maganga wakati wa kikao cha Kikosi kazi kilichoundwa kuratibu zoezi la uanzishwaji wa Benki ya Wananchi Mkoani.

Kwa kushirikiana na sekta binafsi Mkoa wa Kigoma umeanza kutekeleza agizo la Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kasim Majaliwa alilolitoa Mjini Dodoma kuhakikisha Kila Mkoa uwe na Mkakati wa kuanzisha taasisi za kifedha za wananchi yaani Benki ya Wananchi.

Uanzishwaji wa Benki ya wananchi Mkoani Kigoma unalenga kuchochea maendeleo kiuchumi kwakuwawezesha wananchi kupata

huduma za kifedha katika Benki hizo kwa masarti nafuu.

Ni fursa nzuri kwa wajasiriamali na wakulima kuweza kupata mikopo kwa riba nafuu ili kukuza mitaji yao.

Katika kufikia dhamira ya viwanda na nchi ya uchumi wa kati, nilazima kuwepo na mikakati yakuwawezesha wananchi kifedha ili waweze kuwekeza katika viwanda.

Jitihada hizi zitawezekana ikiwa kuna mikakati madhubuti ya uwepo na upatikanaji wa taasisi za kifedha zenye kuwafikia wananchi na kwamasharti nafuu.

Mkuu wa Mkoa amewataka wajumbe wa kikosi kazi kinachoratibu uanzishwaji wa Benki ya wananchi Mkoani Kigoma wafanye kazi kwa moyo na weledi kuwasaidia wananchi na kutimiza dhamira ya serikali kufikia uchumi wa kati na Viwanada.

Mimi nawaambia usipoacha alama yeyote hapa duniani kwa kufanya



**Viongozi wa Mkoa na Wajumbe wa mkutano wa Uanzishwaji Benki ya Wananchi wakifuatilia Mawasilisho ya mada kutoka kwa wataalam.**

matendo mema, kujitoa kuwatumikia wengine kuiko kujijali wewe na maslahi yako wewe huwezi kukumbukwa hata kidogo, nawaomba suala hili mlipe kipaumbele kila siku katika mafikirio yenu. Alimalizia Magaga.





## OPERESHENI ONDOA MIFUGO KUTOKA NJE YA NHI KUFANYIKA MIKOA 12

**W**izara ya Mifugo na Uvuvi imetangaza kufanya operesheni kabambe ya siku 15 ya kuondoa mifugo yote inayotoka nchi za jirani katika mikoa 12 ili-yopo mipakani hapa nchini.

Akizungumza katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Waziri mwenye dhamana na mifugo na Uvuvi Mhe. Luhaga Mpina(MB) amesema wizara yake imejipanga kuondoa mifugo yote ambayo si ya nchi hii ndani ya siku 15 ambapo yeye pamoja na Msaidizi wa Katibu Mkuu wamegawana kusimamia zoezi ilo kwa siku 15.

Ametaja mikoa itakaofikwa na zoezi hilo ni Kigoma, Kagera, Katavi, Kilimanjaro, Arusha na Mara, mikoa mingine ni pamoja na Songwe, Njombe, mbeya

Mhe. Mpina amesema asilimia 30 ya malisho ya Mifugo hapa Tanzania yanatumiwa na mifugo ya wafugaji toka nje ya nchi, jambo linalofanya wafugaji wa ndani kukosa malisho na ardhi ya kulima na hivyo kusababisha migogoro mingi kati ya wafugaji na wakaulima

Sambamba na kuzuia migogoro inayosababishwa na mifugo hiyo amesema kuwa wizara itaweza kudhibiti magonjwa ya mifugo yanayoweza kusababishwa na mifugo inayoingizwa nchinikutoka nchijirani kwa kufuata malisho.

“udhibiti wa mifugo utasaidia pia kuepukahasara kwa serikali na wafugaji wetu kupoteza mifugo yao sababu ya magonjwa, na uchafuzi wa mazingira,



*Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Luhaga Mpina (MB) akisisitiza jambo wakati wa Ziara yake Mkoani Kigoma, aliyekaa ni Mkuu wa Mkoa wa Kigoma Brigedia Jenerali (Mst) Emmanuel Maganga.*

zoezi hili ni kwa mujibu wa sharia ya Mifugo Na. 17 ya mwaka 2013.

Imeelezwa kuwa hatua kali itachukuliwa kwa mifugo hiyo ikipatikana ikiwemo faini au kutafishwa kwa mifugo, amewataka watu walioingiza mifugo nchini kinyemela kuiondoa maramoja kabla ya kupatwa na dhahama hiyo.

Ameagiza kuwa baada ya siku 15 za operesheni kila Mkoa utahakikisha kutoa taarifa za uthibitisho wa kutoingia Mifugo tena kutoka nchi jirani. Aidha, Mhe. Mpina ameagiza Mikoa yote kukamilisha zoezi la upigaji chapa mifugo kukamilika ifikapo tarehe 30 Desemba, 2017

Aye Mkuu wa Mkoa amemhakikishia Waziri kuwa Mkoa upo taari kuhakikisha zoezi la kuondoa mifugo kutoka nje linafannikiwa kwani kumekuwepo na kero ya uingizwaji wa mifugo kutoka Burundi na Rwanda Mkoani humo.



**Mkuu wa Mkoa wa Kigoma Brigedia Jenerali (Mst) Emmanuel Maganga akikabidhi taarifa ya Mkoa kwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Luhaga Mpina (MB)**



# Madiwani na Watendaji watakiwa kuzingatia Mahitaji ya kitalaam ya Mpango Mkakati wa Mji wa Kigoma.

**M**adiwani na watendaji katika Manispaa ya Kigoma Ujiji wame-takiwa kutimiza na kuzingatia masuala ya kitaalamu ya Mpango Mkakati wa maendeleo wa Mji wa Kigoma Ujiji, kwa kuzingatia sheria, ufanisi na kutopindisha mipango jambo linalosababisha migogoro isiyo ya lazima.

wezankujenga popote bila kufuata utaratibu nawaomba wananchi wa Kigoma mlielewe hili" aliongeza Maganga.

Nao wadau mnalimbali walooshiriki katika mkutano huo wametoa maonia yao kwa kusisitiza elimu ya uelewa juu ya masuala ya ardhi inahitajika, kwani bila uelewa wa wananchi bado tatizo la migogoro ya Ardhi litaendelea kuwepo. Wananchi wanatakiwa kuelimishwa hatua zote za upatikanaji wa ardhi namna ya kuuza/kununua ili kuepuka watu zaidi ya mmoja kununua kiwanja kimoja au kununua maeneo ya wazi.

Mpango wa maendeleo wa Mji wa Kigoma Ujiji 2017-2037 umelenga

kuboresha Mji kwa kuondoa tatizo la ukuaji wa mji, ujenzi holela na uvamizi wa maeneo ya uwekezaji na yale ya wazi. Aidha mpango huu utaugharisha mji wa Kigoma ambao unatajwa kuwa ni Mji wa Kimkakati kutokana na fursa mbalimbali za kibiashara, kilimo, na viwanda ambapo katika Nchi za Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Zambia, Mji wa Kigoma ndiyo Lango kuu katika nyanja mbalimbali kiuchumi.



Hayo yamesemwa na Mkuu wa Mkoa wa Kigoma, Brigedia Jenerali (mst.) Emmanuel Maganga wakati wa Mkutano Mkuu wa wadau wa Mji wa Kigoma Ujiji wa Mpango Kabambe wa Maendeleo ya Manispaa hiyo.

Maganga Amesema mpango huu siyo wa kisiasa bali unalenga kuleta tija kwa wakaI wa Mji wa Kigoma Ujiji hivyo tunapaswa kuutekeleza kwa ufanisi mkubwa. Tuwasaidie wananchi kuondoa kero za migogoro ya ardhi.

Ameongeza kuwa watendaji wa serikali kwa miaka iliyopita wamesababisha migogoro mingi ya ardhi kutokana na kutokuzingatia taratibu na sheria, kufanya kazi kwa kukuika mipango kazi ya maendeleo ya Mjiji iliyokuwepo hapo awali.

Aidha upande wa wananchi Brigedia Jenerali (mst.) Maganga amewataka waachenkuuziana nankununua mawneo bila kufuata taratibu za ardhi jambo ambalo linaweza kuwaingizia hasara za kutapeliwa ama kubomolewa majengo yao na serikali." Kuwa na fedha himaniniishinuna-



**Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa wadau wa Mji wa Kigoma Ujiji wa Mpango Kabambe wa Maendeleo ya Manispaa wakifutulia maelezo kutoka kwa wataalam wa Masuala ya Mipango**





## Waziri Luhaga Kupambana na Uvuvi haramu Nchini kufakupona

**K**iamakikubwa kwa, wavuvi haramu na waingizaji wa zana za uvuvi haramu inakuja, Mhe. Waziri Luhaga Mpina ameyasema haya wakati wa Ziara yake ya kikazi Mkoani Kigoma mara baada ya kupokea taarifa ya Mkoa wa Kigoma kuhusu halialisi ya uvuvi katika ziwa Tanganyika.

Amesema aiwezekani vita ya uvuvi haramu inasemwa kila siku halafu haiishi " hivi hii kama ni vita ni vita ya namna gani haina mwisho, mimi kama waziri mwenye zamana nasema siwezi kukubali nikishindwa nitajiondoa katika wadhifa huu". Amesema Luhaga.

Ameeleza kabla ya hajajiondoa lazima wahusika wa uvuvi haramu na watendaji au mtu yeyote awaye mwenye kujihusisha na uvuvi haramu lazima amshughulikie ipasavyo. Hiwezekani serikali ipo, wataalam wapo na vyombo vya ulinzi vipo halafu tuendeleo kuchezeza na watu wachache kwa maslai yao binafsi amesisitiza Mhe. waziri

Mbali na uvuvi haramu kuhatarisha upotevu wa mazalia ya viumbe vya majini, pia umekuwa chanzo kikubwa cha uhatarishi wa afya zetu, magonjwa ya kansa na moyo yanaongezeka kutokana na utumiaji wa sumu, baruti na mabomu kuvua vitoo vya majini

Kwa kipindi cha mwaka 2016/2017 jumla ya Zana haramu zenye kukadiriwa kuwa na thamani ya Shilingi za Kitanzania 480,675,000 ziliteteketwa Mkoani Kigoma ambazo zilikatwa mwambao wa Ziwa Tanganyika.

Zana hizo Kokoro 66, monofilament/timber 173, vyandarua (kokoro) 45, makila ya undersize 47, mitimbo 3, maboksi ya kuhifadhia samaki 8, Kamba Mita 22,500 na samaki wachanga zaidi ya kilo 720.



**Samaki waliovuliwa tayari kwa wachuuzi kuwafikisha kwa watumiaji**

Mhe. Mkuu wa Mkoa amesisitiza kuwa serikali ya Mkoa itaedelea kulin-da rasilimali za Ziwa Tanganyika kwa kusimamia uvuvi edelevu kwa vizazi vijavyo, amewatahadharisha wavuvi na wanannchi kuepukana na vitendo vya uvuvi haramu, ikumbukwe kuwa wavuvi wa zana zote wanapaswa kuzingatia Sheria na kanuni zilizowekwa ili kuhifadhi rasilimali ya uvuvi iwe endelevu na yenye manufaa kwa jamii nzima.



**Mkuu wa Mkoa wa Kigoma Mhe. Brigedia Jenerali (mst.) Emmanuel Magaga wakiongozana na Waziri wa Mifugo Mhe. Luhaga Mpina kukagua Mwalo wa Kibirizi Mkoani Kigoma**



## Wakandarasi barabara ya Kigoma – Nyakanazi Ongezeni kasi

Viongozi mbalimbali Mkoani Kigoma wametaka uwekwe msisitizo mkubwa kwa wakandarasi wanaojenga barabara ya Nyakanazi – Kabingo yenye urefu wa kilomita 54 na Kasulu – Kidahwe yenye urefu wa 63 kwani wanaenda polepole mno.

Viongozi hao wameyasema hayo mbele ya Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi, na Mawasiliano Mhe. Mhandisi Atashasta Ndiye (Mb) katika Kikao cha Bodi ya Barabara ya Mkoa wa Kigoma.

Hii imetokana na taarifa aliyotoa Meneja wa Wakala wa Barabara Mkoa wa Kigoma Mhandisi Narcis Choma ambaye amesema kasi ya Mkandarasasi anayeshughulikia barabara ya Nyakanazi – kabingo Wilayani Kibondo yenye urefu 54km Kasi yake si ya kuridhisha kutokana na Mkandarasi huyo kuwa na vifaa vichache na vibovu. Hadi sasa ni aslimia 35tu ya kazi ndiyo imekamilika ambayo ni kuweka baadhi ya madaraja na kumwaga vifusi.

Kwa mujibu wa taarifa ya wakala wa Barabara Mkoani Kigoma, barabara hizo zilitakiwa zikamilike Mwaka huu mwezi Desemba lakini kutokana na changamoto kadhaa muda umeongezwa hadi mwezi mei mwakani 2018.

Aidha mkandarasi anayejenga barabara ya Kasulu – Kidahwe yenye urefu 63 km nayo inasuasua pamoja na Serikali kutoa fedha zote kwa Mkandarasi huyo.



Viongozi hao wametaka wakandarasi hao waongeze kasi ili kuendana na kasi ya serikali ya awamu ya tano na agizo la Mhe. Rais wa Jamhuri ya



*Mkuu wa Mkoa wa Kigoma Mhe. Brigedia Jenerali (mst.) Emmanuel Magaga akiwa katika Ziara ya Kikazi kukagua Miradi mbalimbali ikiwemo ya miundombinu ya barabara .*

Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Magufuli ambaye aliwataka wakandarasi na Wizara husika kuharakisha ukamilishaji wa barabara hizo muhimu kwa wakazi wa Mkoa wa Kigoma.

Mkoa wa Kigoma kwa miaka mingi umeteseka kutokana nanku-kosekana kwa miundombinu bora ya barabara yenye kuunganisha na Miioa mingine.

*Wakandarasi wakiendelea na Ujenzi wa barabara ya kiwangocha lami Kidahwe— Kasulu 63 km katika hatua ya kuweka madaraja na Makaravati*



## TAKRIBANI BILIONI 32 ZA TASAF ZATUMIKA KWA KAYA MASIKINI MKOANI KIGOMA



Jumla ya Shilingi billion 32 kutoka katika Mfuko wa Maendeleo ya Jamii TASAF zimetumika katika miradi mbalimbali katika kupuguzwa umasikini Mkoani Kigoma, ikiwemo kuziwezesha kaya Masikini.

Haya yameelezwa na Mkuu wa Mkoa wa Kigoma Brigedia Jenerali Emanuel Maganga leo amekutana na kufanya Mazungumzo na mwakilishi wa wahisani wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii TASAF ambaye pia ni mshauri wa masuala ya uchumi katika Ubalizi wa Sweden hapa nchi Bi. True Schedvin.

Akitoa shukrani zake kwa wahisani Maganga amesema anawashukuru kwa moyo wao wa kujitoa kusaidia kupunguza umaskini katika Mkoa wa Kigoma. "Kwa niaba ya wananchi wa Mkoa wa Kigoma tunafarijika na moyo wenu wa kusaidia jitihada za kuondoa umaskini kwa wananchi, tunatambua wazi fedha mnazotoa si ziada kwenu bali ni matashi

mema ya kutaka wananchi wetu hapa Kigoma waondokane na umaskini" aliongeza Maganga.

Mhe. Maganga amemhakikishia Bi. Schedvin kuwa Serikali ya Mkoa wa Kigoma itahakikisha fedha zinazotolewa na wahisani zinasimamiwa kwa malengo yaliyokusudiwa kwa manufaa ya wananchi wa Kigoma na si vinginevyo.

Naye Bi. Schedvin amesema kuwa lengo la ziara yao ni kuangalia, utekelezaji wa miradi mbalimbali ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii pamoja na changamoto zinazojitokeza ili kuweza kuzirekebisha.

Aidha watendaji wamehimizwa kusimamia kwa ukamilifu matumizi sahihi ya fedha za wahisani katika miradi mbalimbali kwa lengo la kabadili maisha ya wananchi wa Kigoma kuondokana na Umaskini.





## RC AHIMIZA KILIMO BORA CHA PAMBA

**M**kuu wa Mkoa wa Kigoma Brigedia Jenerali (mst) Emmanuel Maganga amewahimiza wakulima wa pamba Wilayani Kakonko kulima pamba kwa ubora na kuimarisha ushirika ili kuongeza uchumi kwa kila mtu. Akifanya ziara Wilayani kakonko hivi karibuni kuhasisha kilimo bora cha pamba mhe. Maganga ameeleza kuwa Serikali imetoa ruzuku na bei elekezi kwa mbolea ya kupandia ya DAP ambayo itauzwa Tsh.55741 na mbolea ya kukuzia UREA itauzwa Tsh.43,162. Hapo awali mbolea hizo zilikuwa zikiuzwa kati ya sh.50,000 hadi 80,000.

Aidha ametoa wito kwa wakimbizi wanaoishi nchini Tanzania kuishi kwa amani na watanzania na kuepuka kufanya mauaji na vitendaji vya uporaji. Mkuu wa Mkoa ametembelea kata ya Kasanda, Kanyonza na Kasuga na kuzungumza na wakulima wa pamba ili kuwaeleza mkakati madhubuti wa Serikali kuhakikisha zao la pamba mkoani Kigoma lina-kuwa na tija zaidi na fida kwa wakulima.

Aidha mkuu wa Mkoa amewaagiza Maafisa ugani kulima mashamba ya



mfano ili wananchi waweze kujifunza kupitia mashamba hayo. Wakati huo amesisitiza suala la utii wa sheria bila shuruti ikiwemo kuepuka kilimo cha bangi ambapo mwaka jana 2016 heka 8 za bangi zilikamatwa. Vilevile amewataka wananchi kudumisha ushirikiano na upendo na kuacha ukabila. Ameeleza kuwa baadhi ya wananchi wanajichukulia sheria mkononi kwa kuwaua wazee kwa imani za kishirikina.

**Mkuu wa Mkoa wa Kigoma Mhe. Brigedia Jenerali (mst.) Emmanuel Magaga akipatiwa maelezo kuhusu kilimo cha zao la pamba kutoka kwa wataalam wa Halmashauri ya Wilaya ya Kakonko**



## Waliojenga kwenye hifadhi ya barabara watakiwa kuondoa majengo yao Kigoma



*Kutoka kushoto Mhe. Mhandisi Atashasta Nditiye (Mb) Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi, na Mawasiliano katikati ni Mkuu wa Mkoa wa Kigoma Mhe. Brig. Jen. (mst.) Emmanuel Maganga na Katibu Tawala wa Mkoa wa Kigoma Bw. Charles Pallangyo wakifuatilia mjadala katika Kikao cha Bodi ya Barabara cha Mkoa*

**S**hughuli za kibinadamu, wizi wa vyuma kwenye makaravati na alama za barabarani, utifiri wa viziuzi barabarani, upitishaji holela wa mifugo, magari kuzidisha uzito unaotakiwa na utupaji wa taka kwenye mitaro yabarabara; vimetajwa kuwa vyanzo vikubwa vya uharibifu na uchakavu wa miundombinu ya barabara.

Haya yameelezwa katika kikao cha kwanza cha Bodi ya Barabara ya Mkoa wa Kigoma kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Aidha tatizo jingine limekuwa la wananchi kuongeza ujenzi kwenye hifadhi ya barabara, kuweka miundombinu ya biashara sehemu za barabara kinyume na sheria.

Kufuatia hali hii Meneja wa Wakala wa barabara Mkoa wa Kigoma Mhandisi Narcis Choma ameeleza kuwa jumla ya wafanyabiashara 537 waliojenga mabanda, maduka, ama nyumba zao kwenye maeneo ya hifadhi ya barabara Barabara wanatarajiwa kuondolewa mara moja

Mkoani Kigoma hususan katika Manispaa ya Kigoma ujiji, Kasulu na Kibondo.

Akiongea katika kikao hicho Meneja wa Wakala wa Barabara Mkoa wa Kigoma Mhandisi Choma amesema agizo hili linazingatia Sheria ya Barabara Namba. 13 ya mwaka 2007 ambayo inazuia kujenge, au kufanya biashara ya aina yoyote kwenye hifadhi ya barabara.

Kwa sasa wahusika wanaofanya shughuli mbalimbali katika maeneo ya barabara wamekwishajulishwa kwa utaratibu wa barua, ambapo amewataka wenye karakana za magari, pikipiki na bajaji waanze kuondoa vitu vyao kwa hiyari kabla mamla ya TANROARDS haijaanza kutekeleza zoezi la kuwaondo wahusika ikiwemo kuboboa.